

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



**Namba ya Kotesheni:** LGA/018/2019/2020/NCS/10

Kwa ajili ya:

**KUPANGISHA MADUKA KUMI NA TISA (19) KATIKA ENEO LA DRIMP - ILALA**

**MWALIKO WA KOTESHENI YA UPANGISHAJI**

Tarehe 17/02/2020

1. Mwaliko huu wa Kotesheni unafuata Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa mwaka wa fedha 2019/2020 unaoonekana katika tovuti ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na tovuti ya PPRA.
2. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Halmashauri. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika mwaka wa fedha 2019/2020, inakusudia kupata wapangaji kwa ajili ya kupanga katika maduka kumi na tisa (19) yaliyopo eneo la DRIMP – Ilala, mkabala na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.
3. Waombaji wanakaribishwa kuchukua kabrasha la kotesheni kwa gharama ya shilingi 50,000/ fedha ambazo hazitarudishwa. Waombaji wanatakiwa kufanya malipo kwenye akaunti namba Na. 0150211141600, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, CRDB PLC, kwa ajili ya kupangisha maduka kumi na tisa (19) yaliyopo eneo la DRIMP – Ilala, mkabala na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.
4. Kotesheni zote ziwe na nakala halisi (original) mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa “Kotesheni Na LGA/018/2019/2020/NCS/10 **Kupangisha maduka kumi na tisa (19) katika eneo la DRIMP – Ilala mkabala na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.** Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam S.L.P. 9084 Dar es Salaam, Kitengo cha Manunuzi (PMU).

5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni tarehe **28/02/2020 siku ya Ijumaa saa nane mchana**. Kotesheni zote zitafunguliwa hadharani mara tu, baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa waombaji wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, S.L.P. 9084 Dar es Salaam Kitengo cha Manunuzi (PMU).
6. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.



Sipora J. Liana

**MKURUGENZI WA JIJI  
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**